



KUCHUNGUZA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA WIMBO WA FULL STOP WA TAARAB YA MIPASHO WA KHADIJA KOPA

*Abdulrahman Fayz Baheeri & Mohamed Omary Maguo

Department, Swahili language the faculty of arts and social sciences, Open University, Dar es Salaam, Tanzania

Keywords:

Matumizi
Katika
Kuona
Wimbo

ABSTRACT

Makala haya yanalilenga kuchunguza matumizi ya lugha katika wimbo "Full stop" wa taarab ya mipasho wa Khadija Kopa ili kuona mchango wake katika kuibua dhamira ya mapenzi kwenye wimbo huo wa msanii maarufu ambaye anajulikana kwa jina la malkia wa nyimbo za taarab (Khadija Kopa). Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini pamoja na kusikiliza. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kitaamuli yaani isiyokuwa ya kimahesabu. Makala haya yameongozwa na nadharia ya Simiotiki katika uchmabuzi wa data na kutoa data matokeo yanayoonyesha matumizi ya lugha ya mafumbo, kuchanganya ndimi, matumizi ya mbinu ya sitiari na tashibiha ambazo zote zimetumika kuibua na kujenga dhamira ya mapenzi katika wimbo ulioteuliwa.

التحقيق في استخدام اللغة في أغنية توقف كاملة ل خديجة كوبا في تغذية الطرب

*عبدالرحمن فايز ابخيري الصبي و محمد عمري ماقو

قسم اللغة السواحيلية، كلية الآداب والعلوم الاجتماعية، الجامعة المفتوحة، دار السلام، تنزانيا

الكلمات المفتاحية:

استخدام
أغنية. في
نظر

الملخص

تهدف هذه المقالة إلى دراسة استخدام اللغة في أغنية "نقطة" من موسيقى الطرب لخديجة كوبا لمعرفة مدى مساهمتها في إثارة موضوع الحب في أغنية الفنانة الشهيرة المعروفة بملكة الطرب (خديجة كوبا). تم جمع البيانات لهذه المقالة باستخدام مزيج من تقنيات القراءة الدقيقة والاستماع. تم تحليل البيانات المجمعة باستخدام أسلوب غير كمي. تسترشد هذه المقالة بنظرية السيميائية في تحليل البيانات وتقدم نتائج البيانات التي تظهر استخدام اللغة المجازية وخلق اللغات واستخدام تقنيات الاستعارة والتشبيه، والتي تم استخدامها جميعاً لاستحضار وبناء موضوع الحب في الأغنية المختارة.

1.1 The Utangulizi

Taarab ni tasnia ambayo imepiga hatua kubwa sana ya maendeleo katika jamii za ukanda wa Pwani ya Afrika ya Mashariki kutokana na nafasi yake katika utamaduni wa Mswahili (Yego, 2013). Taarab asilia ndiyo ya kwanza kuingia na kuimbwa katika jamii za Waswahili lakini kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na maingiliano ya jamii moja na nyingine yamesababisha kuibuka kwa mkondo mwingine wa nyimbo za taarab unaitwa taarab ya Mipasho (Juma, 2022, Alhabib, 2012). Hii ni aina ya taarab ambayo imepata umaarufu mkubwa sana katika jamii kutokana na uwasilishaji wake kuwa ni ule unaowavutia zaidi vijana kutokana na vionjo vyake kuwa ni kuzungumzia masuala ya mapenzi waziwazi, lugha ya mazungumzo ya vijana, masuala ya umbeya, fitina, wivu na masuala mengine kama hayo yanaelezwa waziwazi kwa njia ya kutupiana vijembe baina ya watunzi au wake wenza (Abdallah, 2018). Taarab ya mipasho imepata mashiko zaidi katika jamii hasa katika kipindi hiki cha utandawazi kinachochagizwa na soko huria na wasanii wakitumia taarab ya mipasho kama chombo cha kujipatia ajira na fedha nyingi (Askew,

1997). Matumizi ya lugha ni miongoni mwa vipengele vya kifani ambacho kinaifanya taarab ya mipasho kuwa kivutio cha wanajamii na hususani kundi la vijana pamoja na wanawake na ndiyo maana makala haya yameamua kuchunguza kipengele hicho katika wimbo wa "Full Stop," wa taarab ya mipasho wa Khadija Kopa.

1.2 Mkabala wa kinadharia

Nadharia ya makala haya ni Simiotiki ambayo inajihusisha na masuala ya lugha kwa kutazama kile kinachotajwa na namna kinavyotajwa. Kwa maneno mengine, nadharia ya Simiotiki inahusu kitaja na kitajwa ikiwa kitaja ni neno linalotajwa kitu na kitajwa ni kile ambacho kinatajwa kupitia neno husika (Barthes, 1994). Nadharia hii imejengwa katika misimbo mitano ya kihemenitiki, kiishara, kiseme, kiutamaduni na kimatukio (Chandler, 1992). Kupitia misimbo hii ndio mtafiti ama mwandishi wa makala anapoweza kubaini picha, ishara, taswira, misimbo, mafumbo na lugha za kejeli na dhihaka na kuzichambua viziuri kwa namna inayoweza kutimiza lengo la makala husika. Nadharia hii ni muafaka katika uandishi wa makala haya na

*Corresponding author:

E-mail addresses: arhaim1991@gmail.com

Article History : Received 27 April 2025 - Received in revised form 13 October 2025 - Accepted 30 October 2025

imesaidia katika kutimiza lengo la makala la kuchunguza matumizi ya lugha katika wimbo wa “Full stop,” wa taarab ya mipasho wa Khadija Kopa na namna ulivyosaidia kujenga dhamira ya mapenzi.

1.3 Methodolojia ya makala

Makala haya yamekusanya data kwa kutumia mbinu ya udondozi mitandaoni na usomaji makini. Kupitia mbinu ya udondozi wa mitandaoni, mtafiti wa makala haya aliingia katika mtandao wa You Tube na kupakuwa wimbo wa “Full stop,” wa taarab ya mipasho wa Khadija Kopa ambapo mtafiti alifanikiwa kupata wimbo huo uliotoa data za kutimiza lengo la makala haya. Hii ni mbinu mpya ya kukusanya data kutokana na wasanii kuweka nyimbo zao katika mtandao huo. Baada ya kupakuwa wimbo, mtafiti alisoma mashairi ya wimbo husika kwa makini ili kupata data za matumizi ya lugha katika wimbo huo. Kothari (2009) na Kombo na Tromph (2006) wanaeleza kwamba, usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kwa kusoma kwa mazingatio matini iliyoteuliwa ili kuweza kutoa data za utafiti na katika makala haya mtafiti alisoma mashairi ya nyimbo tano alizoziteua. Kimsingi, ili kuweza kupata data, mtafiti alizingatia hatua tano katika usomaji wake makini wa mashairi ya wimbo teule wa Khadija Kopa. Hatua ya kwanza ilikuwa ni mtafiti kusoma mashairi ya wimbo huo bila kudondoa ili kupata uelewa wa jumla kuhusu wimbo huo, hatua ya pili ikawa ni kusoma na kuanza kudondoa sehemu ya mashairi ya wimbo huo wa taarab ya mipasho wenye data za matumizi ya lugha na hatua ya tatu ilikuwa ni kuandaa vichwa na mada ambazo ndizo zitakazopokea madondoo ya data. Hatua ya nne ilikuwa ni kuweka data zinazofanana pamoja na kutenga zinazotofautiana ili kuepuka marudio na hatua ya mwisho ilikuwa ni kupangilia data kwa namna ambayo imewezeshia uchambuzi kufanyika kwa ufanisi na kwa tija.

4.1 Matumizi ya lugha katika taarab ya mipasho

Lugha ndicho chombo ambacho kinatumika katika kubeba maudhui ya kazi ya fasihi na taarab ya mipasho ni moja kati ya kazi za fasihi zilizosheheni matumizi ya lugha (Mbiu, 2022). Matumizi ya lugha katika nyimbo za taarab ni kipengele kipana sana na katika makala haya tumechambua vipengele vichache tu ili kutimiza lengo la makala.

4.1.1 Lugha ya Mafumbo

Matumizi ya mafumbo ni aushi katika fasihi simulizi ambayo huipatia kazi ya fasihi ladha na kukubalika katika jamii. Ingawa yapo maelezo kuwa taarab ya mipasho hueleza mambo waziwazi bila kuficha lakini ni ukweli pia katika baadhi ya mambo yanayoonekana kuwa ni ya wazi ndani yake mna mafumbo. Tuone mfano ufuatao kupitia wimbo wa “Full stop:”

Hamisi Simba wa Mwana Nyamala,
Waambie nakuja eeh,
Wamekataa kona,
Wanakubali penati,
(Kiitikio).

Hio ndio pambe top,
Kwa mara nyingine tena,
Mimi ni mtu wa watu,
Nisojua kunong’ona.

Jamani mapaparazi,
Mtajuta kuniona,
Naingilia mapenzi,
Mnayooleana na bwana,
Nimeanza na mizizi,
Penzi sila mwaka jana ooh,
Hatukuingia juzi juzi,
Aah jiji la Dar-es-salama,
Tumelipandia ngazi,
Tukashuka na milima.
Tumeyapika mapenzi,
Tumbo joto lazizizma

Atakaye jitia bazazi,
Hatujianza usalama
Nitamfanyia kazi,
Na mji atauhama,

Katika wimbo huu tunaona kuna matumizi ya lugha ya mafumbo pale kwenye kiitikio ambapo msanii anaeleza kuwa “wamekataa kona, wamekubali penalty akiwa na maana kwamba wahusika hao

waliopinga mpango fulani ili yeye asifanikiwe kumbe ndio wamemfungulia fursa ya karibu ya kuweza kupata ushindi. Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki tunaona hapa kukijengwa msimbo wa kimatukio kwamba kupata goli kwa njia ya kona siyo kitu rahisi kama kupata goli kwa njia ya penalty. Matumizi haya ya lugha yana maana kwamba, katika maisha watu wasipende kuzuiana katika fursa kwani unaweza kumzuia mtu asipate fursa fulani kumbe ndio umemfungulia njia nzuri na nyepesi zaidi ya kufanikiwa.

4.1.2 Kuchanganya ndimi

Matumizi mengine ya lugha yanayopatikana katika nyimbo za taarab ya mipasho za Khadija Kopa kuchanganya ndimi ambapo kunakuwa na matumizi ya lugha zaidi ya moja katika uwasilishaji wa mashairi ya nyimbo za taarab kupitia wimbo huo huo wa “Full stop:”

Fullstop wote kimya,
Super extra Kigori naongea.
Fullstop wacheni kelele,
Nasi ruhsa kujitetea.
Ole wenu mnaopita,
Njia za panya kunifuatilia.
Mimi ni komando wa kike,
Hala hala nitawalipua.
Tena nalipa bishosti wa ukweli,
Nan’najua kunengua.

Matumizi ya mbinu ya kuchanganya lugha yanajitokeza katika dondoo hili kujenga msisitizo wa dhamira ya kutofuatiliana katika maisha. Hapa wale wanaofuatilia maisha ya wenzao ndio wanaambiwa “Full stop” ikiwa na maana wakome kufuatilia mambo ya watu ambayo hayawahusu. Katika nadharia ya Simiotiki msimbo wa kiutamaduni ndio unaotufundisha kwamba hapa kuna matumizi ya lugha za tamaduni mbili yaani Kiswahili na Kiingereza na imetumiwa hivi kama mbinu ya kisanaa ya matumizi ya lugha kwa madhumuni maalumu ya kutoa msisitizo kwenye dhamira iliyokusudiwa na mwandishi. Vile vile katika dondoo hapo juu tunaona matumizi ya maneno “super extra” ikiwa ni maana kuwa ni zaidi kuliko yaani msanii anajigamba kwamba yeye ni bora kwa mbali sana kuliko hao ambao wanamfuatilia katika maisha yao na hivyo anawataka wakome kumfuatilia. Matumizi ya maneno haya ya kuchanganya ndimi yamefanywa kwa azma ile ile ya kutoa msisitizo wa dhamira inayolengwa katika wimbo husika wa “Full stop.”

4.1.3 Matumizi ya Sitiari

Sitiari ni tamathali ya semi ambayo hutumika katika kulinganisha vitu viwili visivyokuwa na sifa ya kufafana kana kwamba vinafanana haswa bila ya kuwa na tofauti yoyote. Matumizi ya sitiari yanajitokeza katika wimbo wa

Kina dada wa Mombasa,
Na nyie wajanja sana,
Na kina dada wa Zenji,
Kwa kweli wajanja sana,
Mkifika uwanjani,
Macho mnatazama,
Sasa mkitoka nje,
Mnawagombea mabwana.

Kiitikio

Mnawagombea mabwana (haifai),
Mnagombea mabwana,
Eeh eeh usiguse **moto** utakuunguza.

Katika dondoo hili matumizi ya sitiari yanajitokeza katika mshororo wa mwisho kabisa kupitia neno “moto” ambapo msanii anafaninisha mapenzi sawasawa na moto kwa maana kwamba yoyote ambaye atachezea mapenzi ya watu basi afahamu kwamba anachezea moto. Katika hali ya kawada moto huwa ni kitu hatari ambacho husababisha madhara makubwa usipodhibitiwa vizuri. Mtu kuchezea mapenzi ya watu ni sawasawa kabisa na kuchezea moto na inaweza kuwa ni hatari sana ya kuweza hata kusababisha kupoteza uhai wa mtu huyo mwenye kuchezea mapenzi ya watu. Haya tumeyapata kutokana na msimbo wa kiseme wa nadharia ya Simiotiki ambao wenyewe unahusu msimbo unaotengenezwa kutokana na maana nasibishi ya kisemantiki ambayo ni moto kufaninishwa na kitendo cha mtu kuchezea mapenzi ya watu.

4.1.4 Matumizi ya Tashibiha

Tashibiha kama ilivyo sitiari, yenyewe hulinganisha vitu viwili kuwa

vinafanana kwa kutumia viunganishi “kama,” “sawasawa na,” “mithili ya,” nakadhalika. Hii ni tamathali ya semi ambapo kutumika kwake katika fasihi huwa ni kwa ajili ya lengo la kujenga na kuwasilisha dhamira iliyolengwa na msanii wa wimbo husika wa taarab au kazi nyingine ya fasihi. Katika wimbo wa “Full stop,” msanii anaitumia mbinu na mfano ni dondoo lifuatalo:

Tumependana wenyewe,
Maneno maneno ya nini,
Eti Serengeti boy,
Kwani mnataka nini.
Sasa nawaambia,
Kijana yuko makini,
Wala haijati kocha,
Maximo yuko chini.
Haitaji msaada wa jezi,
Kiwanja anacho ndani
Anafyatua vibao,
Kama yuko marekani.

Kiitikio

Kama yuko Marekani (sweetie)
Kama yuko Marekani,
Eeh eeh siguse moto takuunguza

Katika dondoo hili kuna matumizi ya tashibiha ambapo chumba na kitanda kinafananishwa na uwanja wa mpira na tena anatajwa kocha maarufu ambaye aliwahi kuifanya timu ya mpira wa miguu ya Tanzania (Taifa Stars) kufika hatua nzuri katika mashindano mbalimbali ambapo kwa miaka mingi haikuwahi kufika. Vile vile, raha anayopewa mpenzi na mpenzi mwenzake inatajwa kuwa ni raha kama vile wapo Marekani. Hili ni taifa tajiri na lenye nguvu na ushawishi mkubwa duniani ambapo watu wengi hutamani kwenda kuishi huko. Kimsingi, hapa kunajengwa msimbo wa kimatukio kwa kufananisha tukio la mpira wa miguu linapochezwa katika uwanja kuwa ni sawasawa na mapenzi kupitia tendo la ndoa yanayofanywa na wapenzi wawili wawapo chumbani.

5.0 Hitimisho

Makala haya yameangazia matumizi ya lugha katika wimbo wa taarab ya mipasho uitwao “Full stop,” wa msanii Khadija Kopa. Kupitia wimbo huu tumeona umesheheni matumizi ya lugha mafumbo, kuchanganya ndimi, sitiari na tashibiha. Maatumizi haya ya lugha yamesaidia katika kuijenga vizuri dhamira ya mapenzi ambayo inamsawiri mwanamke kwa kiasi kikubwa kuliko mwanamume. Matumizi haya ya lugha yamefanywa kwa kurejelea mwimbo mmoja tu wa Khadija Kopa, jambo linaloashiria kwamba katika nyimbo za taarab ya mipasho za msanii huyu kuna utajiri mkubwa sana mbinu za matumizi ya lugha. Makala zaidi yanaweza kuandikwa kwa kuchunguza matumizi ya lugha katika nyimbo za msanii Khadija Kopa.

MAREJELEO

- Abdalla, A. R. (2018). *Kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo za taarab asilia: Mifano ya nyimbo za Shakila Saidi Khamisi*. Tasinifu ya uzamivu (haijchapishwa). Chuo kikuu huria cha Tanzania.
- Alhabib, E. (2012). “Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Taarab”.Tasinifu ya M.A. Kiswahili (Haijchapishwa), Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Askew, K. M. (1997). *Performing the nation: Swahili musical performance and the production of Tanzanian national culture*. Harvard University.
- Barthes, R. (1966). *Introduction to the Structuralism Analysis of Narratives.Criticism: The Major statements*. Ed. C. Kaplan. New York: St. Martin’s Press, Inc.
- Chandler, D. (1992) *Semiotics: The Basics*. London: Routledge Press.
- Juma, J. (2022). *Matumizi ya mafumbo katika nyimbo za taarab za Siti Binti*. Tasinifu ya uzamivu (haijchapishwa). Pwani University.
- Kombo, D. K., & Tromp, D. L. (2006). Proposal and thesis writing: An introduction. *Paulines Publications Africa*, 5(1), 814–

830.

- Kothari, C. (2009). *Research methodology: methods and techniques*. New Edge International (P) Limited Publishers.
- Mbiu, C. (2022). Matumizi ya lugha yanavyoibua dhamira katika ushairi wa Kiswahili. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 1-16.
- Ramadhani, S. K. (2013). *Usawiri wa mwanamke katika taarab ya mipasho: mfano kutoka nyimbo za Mzee Yussuf Mzee*. Tasinifu ya umahiri (haijchapishwa). Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Yego, K. (2013). *Nafasi ya mwanamke: jinsi inavyotetewa katika nyimbo za taarab za Zanzibar*. Tasinifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi.

KIAMBATANISHO: WIMBO WA FULL STOP

1. Full Stop

Utangulizi. Hamisi Simba wa Mwana Nyamala,
Waambie nakuja eeh,

Wamekataa kona,
Wanakubali penati,

Hio ndio pambe top,
Kwa mara nyingine tena,
Mimi ni mtu wa watu,
Nisojua kunong’ona.

Jamani mapaparazi,
Mtajuta kuniona,
Naingilia mapenzi,
Mnayo peana na bwana,
Nimeanza na mizizi,
Penzi sila mwaka jana ooh,
Hatukuingia juzi juzi,
Aah jiji la Dar-es-salama,
Tumelipandia ngazi,
Tukashuka na milima.
Tumeyapika mapenzi,
Tumbo joto lazizizma

Atakaye jitia bazazi,
Hatujaanza usalama
Nitamfanyia kazi,
Na mji atauhama,

Bili ya hongwe jesi kama pamoja salam klabu
twende sasa,

Fullstop wote kimya,
Super extra Kigori naongea.
Fullstop wacheni kelele,
Nasi ruhsa kujitetea.
Ole wenu mnaopita,
Njia za panya kunifuatilia.
Mimi ni komando wa kike,
Hala hala nitawalipua.
Tena nalipa bishosti wa ukweli,
Nan’najua kunengua.
Kanipenda kanizimikia,
Kweli na hasa pale ninaporembua.
Sasa wezi wa mabwana,
Nawaambia ntawachakachua.
Nawapa onyo fullstop,
hii ni challenge full gear
Nye taipu zenu za vichochozoni,
Ndizo zinazo wafaa.
Sio wangu mimi chumba na varanda
Tena ghorofani nampandia

Rama papa Yusuf mtoto wa mama Chichi Mwananyamala,
Heri kuvaa kanda mbili kuliko mdundo mbovu.

Fullstop jipange upya,
Hapa kwangu umechemka.
Mimi nina ladha tamu sana,
Ooh ndio maana hataki kutoka.
Hata mje na waganga lori nzima,
Himaya yangu keshafika.
Mlilie mizimu na makafara,
Na mchinje hata paka.
Fullstop jipangeni upya,
Hapa kwangu mmechemka
Mimi nina ladha sweet sana,
Ooh ndio maana hataki kutoka
Hata mje na waganga lori nzima,
Himaya yangu keshafika.
Mlilie mizimu na makafara,
Na mchinje hata paka.
Ala wajifanya unalipa,
Hutafuti wako ukamweka
Wewe huwezi milki yangu,
Baby cute wa Kiafrika
Kwanza niko pekeyangu,
Nimetulia sina shaka.
Nimetulia na mume wangu,
Mtoto wa Kiafrika.

(Sweete chafarali Bwagamoyo mtoto wa Kikwete)

Ala wajifanya unalipa,
Hutafuti wako ukamweka
Wewe huwezi milki yangu,
Baby cute wa Kiafrika,
Kwanza niko pekeyangu,
Nimetulia sina shaka,
Nimetulia na mume wangu,
Mtoto wa uhakika,
Vikarolaiti vyenu,
Vinavyo wapa jeuri,
Hivyo vikarolaiti vyenu,
Tavipiga marufuku hapa
Mimi nina rangi yangu,
Sitaki uso wa vibaka,
Mimi nina rangi yangu,
Na tena bado nawaka
Vikarolaiti vyenu,
Vinavyowapa jeuri,
Hivyo vikarolaiti vyenu,
Tavipiga marufuku hapa.
Mimi nina rangi yangu,
Sitaki uso wa vibaka,
Mimi nina rangi yangu,
Ni Kopa na bado nalipa.

Kiitikio

Bandika bandika,
Mimi nabandua
Nimekuzidi maarifa,
Huna unalolifanya.
Bandika bandika,
Mimi nabandua.
Tumependana wawili,
Wewe unajivumbika.
Hakutaki pesambili,
Hujijui taka taka.
Bandika bandika,
Mimi nabandua

Maneno Tulika Thabiti Abdul Professional,
Keyboard Tanzania number one,
Mfalme wa keyboard,
Onyesha, onyesha.

Sema sema Musa Musa Musa,
Mipango mfalme wa base Tanzania,
Wamekwama kwa nta,

Raisi wa Mbagala Kaisi Musa Kaisi,
Mwambie asiyaache ya mbaya,
Kuvaa koti nyeupe sio wote madaktari,
Wengine wauza nyama
Eriko Sound Club Tetemeko (Wakaonge)

Fullstop Ochinga nambari one,
Said Mpinduka
Mkono wa shetani hauwingiki,
Watapata taabu sana,
Heheheya Thabiti Abdul,
Mtoto kwa Ilala ahaa,
Mfalme wa keyboard waambie,
Saida mama lukuchikwa,
Almato Senti mala waambie
Tuti mtoto wa Mombasa.

Tumependana wenyewe,
Maneno maneno ya nini,
Eti Serengeti boy,
Kwani mnataka nini.
Sasa nawaambia,
Kijana yuko makini,
Wala haijati kocha,
Maximo yuko chini.
Haitaji msaada wa jezi,
Kiwanja anacho ndani
Anafyatua vibao,
Kama yuko marekani.

yuko Marekani (sweetie)

Kiitikio

Kama

Kama yuko Marekani,

Eeh eeh siguse moto takuunguza